# Taarifa kwa Vyombo vya Habari

*Septemba 6, 2023*

**UZINDUZI WA KAMPENI YA ACTIONAID KUHUSU HAKI YA MABADILIKO YA TABIANCHI**

**#FADHILIKESHOYETU**

Ndugu wana Habari,

Karibuni katika Mkutano wa ACTIONAID TANZANIA pamoja na wadau kutoka mashirika mbali mbali.

Ndugu wana habari,

Lengo la mkutano huu ni kuzindua kampeni ya shirika la ActionAid kuhusu Mabadiliko ya Tabia nchi sambamba na ripoti ya utafiti ya ActionAid iitwayo *“How financial flows: The banks fueling Climate Crisis”* .

Kampeni hii ni ya miaka 3 ambayo imejikita katika kuelimisha jamii kuhusu madhara ya mabadiliko ya tabianchi, kuwajengea uwezo bora wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na kushawishi taasisi za umma na binafsi kuwekeza fedha kwenye kilimo Ikolojia na nishati mbadala BADALA ya kuwekeza kwenye kilimo kinachotumia pembejeo za viwandani na kemikali ambazo siyo rafiki kwa mazingira, na nishati ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa hewa ukaa.

Aidha, ripoti ya ***‘’HOW FINANCE FLOWS: The Banks fueling The Climate Crisis”*** imefichua namna mabenki yanavyochochea mabadiliko ya tabia nchi duniani kama ifuatavyo:-

- Mabenki yameweza kufadhili viwanda vinavyotumia nishati zenye madhara ya kimazingira katika nchi zinazoendelea kwa wastani was dola za kimarekani trioni 3.2 kwa kipindi cha miaka saba tangu kupitishwa kwa mkataba wa Paris.
- Vilevile Mabenki yamefadhili makampuni makubwa ya kilimo cha kibiashara kwa kiasi cha dola za Kimarekani Billion 370 kwa kipindi hicho hicho.
- Mabenki yametoa msaada wa kifedha kwa ajili ya shughuli za viwanda na kilimo cha kibiashara ambacho hutumia pembejeo za kemikali katika nchi zinazoendelea mara 20 ZAIDI ya uwekezaji ulioelekezwa kwenye jitahada za kupambana na madhara yatokanayo na madadiliko tabianchi

Kwa mara ya kwanza, ripoti hii inaonyesha kwa namna gani mabenki makubwa duniani ikiwa ni pamoja na HSBC, Citigroup na Barclays na JP Morgani ambavyo yamekuwa yakifadhili kwa kiwango kikubwa na cha kushangaza, mara 20 zaidi katika visababishi vikuu vya mabadiliko ya tabianchi KULIKO ufadhili katika suluhisho la mabadiliko ya tabia nchi. Mabenki inabidi yatambue kuwa shughuli za kilimo na viwanda wanavyo fadhili katika ukubwa huu vina sababisha madhara makubwa kwa jamii za nchi za Afrika, Asia na Latin America.

**Shirika la ActionAid**
*ActionAid ni shirikisho la kimataifa linalofanya kazi na zaidi ya watu milioni 15 wanaoishi katika nchi Zaidi ya 40 maskini zaidi duniani. Tunataka kuona ulimwengu wenye haki, na Dunia endelevu ambamo kila mtu anafurahia haki ya maisha ya heshima na uhuru bila umasikini na ukandamizaji. Tunafanya kazi ili kufikia haki ya kijamii na usawa wa kijinsia na kutokomeza umaskini.*

Madhara hayo nipamoja na ukosefu wa ardhi, uharibifu wa misitu, uchafuzi wa maji na mabadiliko ya tabia nchi.

**Kwa hiyo,***"Mabenki yanapaswa kujikita katika kukabiliana na madhara yanayoikumba jamii na dunia kwa ujumla, na kuacha mara moja kufadhili uharibifu unaosababishwa na nishati zinazozalisha hewa ukaa na kilimo cha mashamba makubwa kinachotumia pembejeo za viwandani na zenye kemikali haribifu. "*

Ripoti hii inapendekeza njia mbadala, kama vile nishati mbadala na kilimo hai/Ikolojia tena zisimamiwe na kuendeshwa na wanawake na vijana. Lakini lazima juhudi hizi ziungwe mkono na kufadhiliwa na rasilimali za umma. Kilimo ikolojia ni stahimilivu kwa mabadiliko ya tabianchi na kina manufaa makubwa sana ya kimazingira, utamaduni na uchumi hii ikiwa ni pamoja na utatuzi wa matatizo ya upungufu wa maji, usalama wa chakula na umasikini.

**Hivyo basi, ripoti hii ya ActionAid inahimiza yafuatayo:**

I. Mabenki yaache mara moja kufadhili makampuni yote yanayo anzisha miradi ya kukata na kuteketeza misitu, uchimbaji wa makaa ya mawe, kilimo kinachotumia pembejeo haribifu, na upanuaji au uendelezaji wa miradi ya aina hii, ikiwemo usitishaji wa miradi inayoendelea.
II. Mabenki yatunge sera za ndani zinazo linda haki za binadamu na kuzuia uharibifu misitu.
III. Serikali katika ngazi zote lazima zisimamie na kutoa miongozo kwa mabenki na sekta ya fedha kuwataka waache kufadhili undelezaji wa miradi inayotumia nishati zinazozalisha hewa ukaa, na kuendeleza mipango inayolenga kuanzisha na kuendeleza matumizi ya nishati mbadala na kilimo ikolojia.

**==MWISHO==**

**Dokezo kwa wahariri:**
*Utafiti uliofanywa ulishirikisha shirika huru la utafiti la Profundo*

**Kumbuka**:
*Ripoti hii unaweza ipata kupitia tovuti yetu:*
*https://tanzania.actionaid.org/publications/2023/how-finance-flows-banks-fuelling-climate-crisis*

**Kwa Mawasiliano zaidi:**
*Ofisi ya habari ya ActionAid*
*Barua pepe: media-enquiries@actionaid.org*
*Simu:+44 7586107955.*

*Mkurugenzi ActionAid Tanzania*
*Barua pepe: admin.tanzania@actionaid.org*
*Simu: +255 754 744 443*

**Report**

**Press**

**Shirika la ActionAid**
*ActionAid ni shirikisho la kimataifa linalofanya kazi na zaidi ya watu milioni 15 wanaoishi katika nchi Zaidi ya 40 maskini zaidi duniani. Tunataka kuona ulimwengu wenye haki, na Dunia endelevu ambamo kila mtu anafurahia haki ya maisha ya heshima na uhuru bila umasikini na ukandamizaji. Tunafanya kazi ili kufikia haki ya kijamii na usawa wa kijinsia na kutokomeza umaskini.*